**MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA GUCHA KUSINI**
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya

102/3
**KISWAHILI**
FASIHI YA KISWAHILI
**Julai / Agosti 2016**
Muda: Masaa 2½

**1. LAZIMA : SEHEMU YA 'A'**
**HADITHI FUPI**
**Damu Nyeusi na Hadithi nyingine** : ***Ken Walibora na Said A. Mohamed***

**1.** Matatizo yanayolikumba bara la Afrika yanaweza kusuluhishwa kwa njia zipi?
Jadili kwa kurejelea Diwani ya *Damu Nyeusi.*

**SEHEMU YA B**
**TAMTHILIA:**
**Mstahiki Meya** ***: Timothy M. Arege***
**Jibu swali la 2 au la 3**

**2.** "Jina si Kitu. Tumbo ndilo muhimu. Tumbo lako na jamaa yako."
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Fafanua jinsi tumbo limewekwa mbele ya jina katika tamthilia hii. (alama 16)

**3.** Thibitisha ukweli wa msemo kuwa: Sikio la kufa halisikii dawa kwa mujibu wa Tamthlia ya *Mstahiki Meya.* (alama 20)

**SEHEMU YA C**
**RIWAYA:**
**Kidagaa kimemwozea** ; ***Ken Walibora***
**Jibu swali la 4 au la 5**

**4.** "Wachache hawa hawaogopi, ashakum si matusi, hata kutema mate au kumwaga mkojo usoni mwa haki, usawa na uhuru ulipiganiwa na kumwagiwa damu . . . ."
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Kwa kutoa ithibati onyesha mbinu ya lugha iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
c) Thibitisha kwa kutoa mifano saba namna haki za kibinadamu zimekiukwa katika riwaya ya *Kidagaa kimemwozea.* (alama 14)

**5.** Wananchi wa Tomoko wamesalia katika ndoto ya uhuru. Dhihirisha ukweli wa kauli hii. (alama 20)

**SEHEMU YA D:**
**USHAIRI**

**6.** Tohara kwa mwanamke, ni hatari,
Madhara, kwa wake uke, hushamiri,
Hasara, yake peke yake, hudhihiri,
Zinduka!

Epuka, hao ngariba, wajuaji
Hufika, navyo viroba, wachinjaji
Kumbuka hawana tiba wauaji
Amka!

Kiwembe, kilichochafua, na kibutu,
Viumbe, huathirika, ni kwa kutu,
Siombe, yakakufika, mwana kwetu,
Zinduka!

Maradhi, hujitokeza, ya vidonda,
Yaridhi kujichomoza pepopunda,
Na hedhi, hukuchagiza, ikavunda.
Amka!

Isiwe, wembe mmoja, wengi wari,
Ujuwe, Ukimwi huja, ni hatari,
Na iwe, katu si hoja, kuwa mwari,
Zinduka!

Wacheni, mila dhaifu, zinotesa

for more free kcse past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

Kwepeni, amali chafu, nawasa.
Shikeni, uadilifu, tangu sasa,
Zinduka!

(Kutoka: Diwani ya wasakatonge, Muhammed Seif Khatibu, OUP Dares Salaam) Uk 2.

1. Shairi hili ni la bahari gani? Tetea jibu lako. (alama 4)
2. Mshairi antoa mwito gani katika ubeti wa pili? (alama 4)
3. Fafanua msimamo wa mshairi kuhusu tohara. (alama 4)
4. Andika ubeti wa sita kwa lugha ya nathari. (alama 3)
5. Taja na utolee mifano mbinu zozote mbili zilizotumika katika shairi. (alama 4)
6. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi. (alama 2)
   i)Hushamiri
   ii)Kibutu
   iii)Idhilali
   iv)amali.

**SEHEMU YA E:**

**FASIHI SIMULIZI**

**Jibu swali la 7 au la 8**

**7.** a) Eleza mafunzo matano yanayotolewa na methali za Kiswahili. Kwa kila funzo andika methali moja. (alama 10)
   b) Fafanua dhima ya utanzu wa nyimbo katika jamii. (alama 10)

**8.** a) Maigizo ni nini? (alama 2)
   b) Fafanua sifa zozote tatu za maigizo. (alama 6)
   c) Eleza tofauti kati ya ngoma na ngomezi. (alama 4)
   d) Fafanua hasara tatu za miviga na namna ya kusuluhisha hasara hizo. (alama 6)
   e) Tofautisha kati ya mighani na maghani. (alama 2)

for more free kcse past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479